



**CHUO KIKUU CHA AFYA  
NA SAYANSI SHIRIKISHI, MUHIMBILI**

---

**HOTUBA ZA MAHAFAI YA KUMI  
YA CHUO KIKUU CHA AFYA NA  
SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI**

---





**CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI  
MUHIMBILI**



**CHUO KIKUU CHA AFYA  
NA SAYANSI SHIRIKISHI, MUHIMBILI**

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA BARAZA LA  
CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI  
MUHIMBILI,  
BI. MARIAM J. MWAFFISI  
KATIKA MAHAFAJI YA KUMI  
YA CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI  
MUHIMBILI**

**3 DESEMBA 2016**

*Mheshimiwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Al-Haj Dk Ali Hassan Mwinyi,*

*Katibu Mkuu, Wizara Ya Elimu, Sayansi na Tekinologia, Maimuna Tarishi*

*Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Ulisubisya Mpoki,*

*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Profesa Ephata Kaaya,*

*Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Muhammad Bakari,*

*Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu na Wakuu wa Vyuo Vikuu Vishiriki Mlioko hapa,*

*Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili,*

*Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika mbalimbali ya Kimataifa,*

*Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Lawrence Museru,*

*Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Dk. Othman Kiloloma,*

*Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage,*

*Viongozi wa Serikali,*

*Wageni waalikwa,*

*Maprofesa na Wahadhiri,*

*Wahitimu,*

*Wazazi na Walezi,*

*Jumuiya ya Wanachuo,*

*Mabibi na Mabwana,*

## **Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,**

Kipekee kabisa natanguliza shukrani zangu za dhati kwako Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, kwa kuwa nasi leo na kukubali kuwatunukia stashahada na shahada mbalimbali wahitimu wetu wa mwaka huu. Ni furaha yangu kubwa kwa niaba ya Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Uongozi wa Chuo na Wanajumuia wote wa Chuo kukukaribisha kwenye hafla hii ya mahafali ya kumi ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Karibu sana.

Aidha napenda kuwakaribisha wazazi, walezi, ndugu, jamaa na marafiki wa wahitimu, bila kuwasahau viongozi mbalimbali wa Serikali, Mabalozzi, pamoja na Viongozi wa taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa.

## **Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,**

Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuniteuwa kuwa mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Nimeupokea uteuzi huu kwa moyo mkunjufu. Kipekee kabisa napenda kumpongeza Mhe. Rais katika juhudi zake za kusimamia utendaji kazi serikalini na kumaliza mwaka mmoja tangu ateuliwe kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mafanikio makubwa na juhudi zake zinaleta matumaini makubwa ya kurudisha maadili na uwajibikaji katika nyanja zote za kijamii na kiuchumi. Pili napenda kumpongeza Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili aliyemaliza muda wake Bwana Deogratias Ntukamazina na Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Ephata Kaaya kwa uongozi wao mzuri uliowezesha Chuo kufika hapa tulipo sasa kimaendeleo na kufaulu ukaguzi uliofanywa na Baraza la pamoja la Madaktari na Madaktari wa Kinywa na Meno la Afrika Mashariki {*East African Community (EAC) Joint Medical and Dental Practitioners Councils/Boards*} tarehe 14 Machi 2016. Naahidi kuendelea kufanya kazi na Uongozi wa Chuo ili kuhakikisha kwamba changamoto zilizoainishwa kwenye ripoti hiyo zinapatiwa ufumbuzi ili Chuo kiweze kutimiza malengo yake na kushika nafasi ya juu zaidi katika ukaguzi utakaofuata.

## **Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,**

Naomba nichukue nafasi hii vile vile kuwapongeza wahitimu wote wa mwaka huu kwa kufaulu masomo yao vizuri na kutuwezesha sisi sote

kusherehekea siku ya leo. Kipekee kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati na pongezi kwa Maprofesa, Wahadhiri pamoja na wafanyakazi wote wa Chuo na wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Mifupa (MOI), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete kwa michango yao iliyowezesha kupata wahitimu hawa.

Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali, Mashirika ya ndani na nje ya nchi, Vyuho Vikuu washirika wa ndani na nje ya nchi pamoja na watu binafsi kwa michango yao ambayo imekiwezesha Chuo hiki kutekeleza majukumu yake katika nyanja za ufundishaji, utafiti na kutoa huduma kwa jamii. Sherehe hii ya mahafali ni uthibitisho dhahiri wa mchango wao mkubwa katika utekelezaji mzuri wa majukumu ya Chuo.

### ***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,***

Dira ya Maendeleo ya Taifa (*Vision 2025*) pamoja na malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano yanalenga kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Malengo haya hata hivyo yanakumbana na changamoto mbalimbali hususani katika sekta ya Elimu na Afya ambazo kama hazitapatiwa suluhu zitadumaza maendeleo hayo. Kwa kulitambua hilo Chuo kinajitahidi kuanzisha programu mbalimbali zenye uhitaji katika jamii na zinazolenga kuzalisha wataalamu watakaokabiliana na changamoto hizo.

Vile vile Chuo kinatambua kwamba bila kutayarisha wasomi wenye fikra za kimaendeleo na wenye mioyo ya ushindani, malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa hayawezi kufikiwa. Hivyo basi, Chuo kitaendelea kutekeleza mitaala inayosisitiza uwezo wa wahitimu kutekeleza kwa vitendo majukumu yao (*competency based curricula*), na wenye ari ya kulinda heshima ya Mwanadamu na kujiendeleza katika fani zao. Hii inaendana na malengo mahususi ya sera ya Elimu ya Mwaka 2014 inayosisitiza elimu ya mafunzo yenye viwango vya ubora vinavyotambulika kitaifa, kikanda na kimataifa. Vile vile mitaala hii inakidhi moja ya malengo ya Mpango Mkakakati wa Sekta ya Afya (*Health Sector Strategic Plan 2015-2016*) unaolenga kuongeza ubora wa huduma za afya katika ngazi zote. Ni matumaini yetu kwamba wahitimu wanaotokana na mitaala hii watakidhi malengo ya sera hizi mbili.

### ***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,***

Mpango Mkakati wa Rasilimali watu katika sekta ya afya (Human Resource For Health Strategic Plan 2014-2019) unaonyesha kuwa kwa sasa uwiano wa watu kwa daktari mmoja katika mikoa mingi ya Tanzania ni kati ya watu 30,000 mpaka 50,000. Uwiano huu ni mzigo mkubwa kwa daktari na unaweza kupelekea utoaji wa huduma ulio chini ya kiwango. Chuo kitaendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na wadau wengine ili kuhakikisha Kampasi ya Mloganzila inakamilika na kuanza kufanya kazi mapema iwezekanavyo. Ni imani yetu kwamba hii Kampasi ikianza kufanya kazi, Chuo kitaweza kuzalisha wataalamu wa kutosha kukabiliana na upungufu huu. Tunatoa wito kwa serikali na wadau wengine kukisaidia Chuo kuhakikisha kwamba majengo na miundombinu mingine inakamilika mapema ili hospitali iweze kutumika kama ilivyokusudiwa na vile vile kupanua udahili wa wanafunzi wa fani za afya.

Pamoja na jitihada hizi za Chuo uchambuzi ulioainishwa katika Mpango Mkakati wa Rasilimali watu katika sekta ya afya unaonyesha kuwa asilimia 63 tu ya wahitimu wanaojiriwa wanaenda kufanya kazi kwenye vituo walivyopangiwa. Tunaiomba serikali na wadau wa afya kutatua changamoto zinazofanya wahitimu wasiende sehemu wanazopangiwa, ili kufikia kwa haraka azma ya serikali ya kuhakikisha kuwa watanzania wanapata huduma za afya zenye ubora pale wanapozihitaji.

### ***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,***

Ili kuhakikisha kwamba Chuo kinatoa wahitimu wenye viwango vya juu katika kutoa huduma za afya, ni lazima Chuo kiwe na wanataaluma wa kutosha kukabiliana na ongezeko tarajiwa la wanafunzi. Kwa sasa Chuo bado kina uhaba mkubwa wa wanataaluma. Uhaba huu usipotatuliwa mapema itakuwa vigumu kwa Chuo kuongeza idadi ya wanafunzi hata kama kampasi ya Mloganzila ikikamilika inavyotarajiwa. Hivyo basi napenda kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa Serikali na wadau wengine wa maendeleo kukisaidia Chuo kiweze kuajiri wanataaluma wakutosha na wenye ubora ili Chuo kiweze kutoa wataalamu wa kutosha na wenye uwezo wa kufanya kazi walizosomea.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Nne na ya Tano kwa kuwezesha kukamilika ujenzi wa hospitali ya kisasa ya Chuo, yaani *MUHAS Academic Medical Centre* katika Kampasi ya Mloganzila. Hospitali hii muhimu kwa Chuo na kitaifa ambayo ujenzi wake

umeshakamilika kwa kiasi kikubwa itatatua matatizo ya miundombinu ya kufundishia mafunzo kwa vitendo, tafiti na huduma bora za matibabu kwa wananchi. Ni matumaini yangu kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo mengine mbalimbali na miundombinu mingine inayohitajika ili kukamilisha ujenzi wa Kampasi ya Mloganzila.

### ***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,***

Moja ya majukumu ya sekta ya afya yaliyoainishwa katika Mpango wa Kukuza Uchumi na kupunguza umasikini Tanzania (MKUKUTA) ni kuhakikisha kwamba watanania wanakuwa na afya zinazowawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Hata hivyo ili kufikia lengo hilo kuna changamoto nyingi. Chuo kupitia wataalamu wake kinafanya na kitaendelea kufanya tafiti mbalimbali zinazolenga kutatua changamoto hizo. Ni matumaini yetu kuwa serikali itatoa kipaumbele kugharamia tafiti hizo, kwa kuwa siyo kila tafiti zinazotatua changamoto za watanania zimo katika vipaumbele vya wafadhili wa nje.

### ***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,***

Ili kutoa mchango wa kuiwezesha Tanzania kutimiza Malengo ya Milenia ambayo hayakutimizwa na hivyo kuendelezwa katika Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals 2016- 2030*). Chuo kinaendelea kutia mkazo katika kutoa elimu bora kwa wahitimu wake kwa kuhakikisha kwamba kuna sera na miongozo stahiki ya kusimamia ubora wa elimu (*quality education*) hapa Chuoni. Kwa mtazamo huu, Chuo kilianzisha Kurugenzi ya Kusimamia Ubora wa Huduma zinazotolewa Chuoni (*Directorate of Quality Assurance*). Kwa misingi hii, ni matumaini yetu kwamba Chuo kitatoa mchango mkubwa zaidi katika kutoa elimu bora kwa wataalamu wa afya nchini, na hivyo kutoa mchango kubwa katika kuiwezesha Tanzania kutimiza lengo la tatu la Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals 2016- 2030*), yaani Afya Bora na Usitawi wa Watanania.

### ***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,***

Napenda kuwakumbusha wahitimu wa leo ukweli kuhusu maisha ya kitaaluma: Kwamba, maisha na mitazamo ya watanania wengi yanabadilika kila wakati kwa misukumo mbali mbali itokayo kwenye mitandao ya kijamii. Lakini utendaji uliotukuka wenye tija, uletao maendeleo unaotokana na msukumo wa sayansi na teknolojia. Ni



jukumu la kila mhitimu kuukubali na kuuchangamkia zaidi msukumo wa sayansi na teknolojia kuliko misukumo mingine iliyozagaa kwenye mitandao ya kijamii. Hii itasaidia kuleta maendeleo ya haraka kwa mhitimu mwenyewe, familia yake na taifa kwa ujumla. Ikumbukwe dhahiri kwamba, maendeleo hayaji kwa nasibu, bali kwa mchakato unaohitaji kujitoa, na kujinyima kwa faida ya kesho. Kila mmoja anafaa akumbuke methali isemayo “*Mchumia juani, hulia kivulini*”. Vile vile kwa upande wa wanafunzi ambao hawajahitimu, nawaasa kusoma kwa bidii ili watakapohitimu wawe na weledi wa kutosha katika fani zao. Kwa sababu historia inaonyesha kwamba, wanaohitimu bila weledi huwa ni wafanyakazi wenye kutojiamini, na kutojiamini kazini husababisha ufanisi usio na ubora, tija na kukwaza maendeleo. Nisingependa wahitimu wa Chuo hiki chenye historia na uzoefu wa muda mrefu katika kufundisha masomo ya fani za afya wawe wasiojiamini katika kazi zao za kuhudumia watanzania.

Kwa kumalizia napenda kuwapongeza tena wahitimu wote kwa kufaulu mitihani yao. Nawatakieni kila la kheri na mafanikio katika maisha na shughuli zenu za baadaye.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, wageni waalikwa, mabibi na mabwana, Ahsanteni sana kwa kunisikiliza!***

**Mwisho**

**CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI  
MUHIMBILI**



**CHUO KIKUU CHA AFYA  
NA SAYANSI SHIRIKISHI, MUHIMBILI**

**HOTUBA YA MAKAMU MKUU WA CHUO KIKUU CHA AFYA  
NA SAYANSI SHIRIKISHI – MUHIMBILI, PROFESA EPHATA  
KAAYA KWENYE MAHAFAZI YA KUMI YA CHUO**

**TAREHE 3 DESEMBA 2016**

*Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Al-Haj Dk Ali Hassan Mwinyi,*

*Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Bi. Mariam J. Mwaffisi,*

*Katibu Mkuu, Wizara Ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Bi. Maimuna Tarishi*

*Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Mpoki Ulisubisya,*

*Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Muhammad Bakari,*

*Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili,*

*Makamu Wakuu wa Vyuo Vukuu na Wakuu wa Vyuo Vikuu Vishiriki Mlioko hapa,*

*Mabalizi na Wawakilishi wa Mashirika mbalimbali ya Kimataifa,*

*Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifu Muhimbili, Profesa Lawrence Museru,*

*Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Dk Othman Kiloloma,*

*Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage,*

*Viongozi wa Serikali,*

*Wageni waalikwa,*

*Maprofesa na Wahadhiri,*

*Wahitimu,*

*Wazazi na Walezi,*

*Jumuiya ya Wanachuo,*

*Mabibi na Mabwana,*

Kwa niaba ya Wanajumuia wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, ninayo heshima kubwa kukukaribisha Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, kwenye mahafali haya ya **kumi** tangu Chuo hiki kiwe Chuo Kikuu kamili. Napenda pia kukushukuru kwa kukubali kuja kuwatunukia stashahada na shahada mbalimbali wahitimu wa mwaka huu.

Aidha napenda pia kuwakaribisha na kuwashukuru wageni waalikwa, viongozi wa Serikali, viongozi wa taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za kiserikali, mabalozi, wazazi, walezi, ndugu na marafiki kwa kukubali mwaliko wa kushiriki nasi katika sherehe hii ya mahafali. **Karibuni sana.**

### **Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,**

Awali ya yote, napenda kuungana na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, kumpongeza Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk John Pombe Joseph Magufuli katika juhudi zake za kupambana na ufasadi. Pia napenda kumpongeza Bi. Mariam Joy Mwaffisi, kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza La Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Nawatakia baraka za Mwenyezi Mungu katika kutekeleza majukumu yao. Pia napenda kumshukulu Mwenyekiti wa Baraza la Chuo wa kwanza aliyemaliza muda wake, Bwana Deogratias Ntukamazina kwa juhudi na utendaji wake wa kazi uliotukuka, katika kipindi chote amabcho alikuwa Mwenyekiti wa baraza la Chuo na kuweza kukifikisha Chuo hapa tulipo leo.

### **Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,**

Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wahitimu wote wa mwaka huu kwa kufaulu vizuri masomo, licha ya changamoto mbalimbali za kitaaluma na kijamii katika kipindi cha masomo yao. Ni imani yangu kwamba wahitimu wa mwaka huu mtakuwa mabalozi wazuri wa Chuo hiki chenye sifa nzuri kitaifa na kimataifa, kwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa na kuzingatia weledi na miiko ya taaluma zenu.

Mafanikio yaliyofikiwa leo na wahitimu hawa yasingeweza kupatikana bila ya mchango mkubwa wa Serikali, Maprofesa, Wahadhiri, wafanyakazi wote wa Chuo na wafanyakazi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete - Muhimbili, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Hospitali ya Jeshi Lugalo na wale wa Hospitali na Taasisi nyingine za afya zinazoshirikiana na Chuo katika kuwaandaa wahitimu hawa na kufanikisha siku hii ya leo. Hawa

wote pia wanastahili shukrani zetu na pongezi nyingi.

### **Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,**

Baada ya kusema hayo, napenda sasa kuchukua nafasi hii kuwatambulisha kwako wahitimu wa mahafali ya leo ambao muda si mrefu utawatunukia shahada ya uzamivu, shahada za uzamili, shahada za kwanza, stashahada za juu na stashahada mbalimbali za Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili.

Mwaka huu wa masomo Chuo kina jumla ya wahitimu **944** kati ya hao **372** wakiwa ni wahitimu wa kike ambao ni asilimia **39.4** ya wahitimu wote. Azma ya Chuo ni kuwa na asilimia sawa kati ya wahitimu wa kike na wa kiume. Hivyo basi Chuo bado kinaendelea na mpango wake wa kuwawezesha wanafunzi wa kike kujiunga na programu mbalimbali zinazotolewa hapa chuoni.

Aidha katika wahitimu wa mwaka huu, **376** watatunukiwa stashahada na **8** watatunikiwa stashahada za juu katika fani mbalimbali za afya na sayansi shirikishi. Pia wahitimu **367** watapata shahada ya kwanza na wengine **183** shahada ya uzamili. Vile vile wahitimu **wawili** watatunukiwa Digrii za Uzamili za Utaalamu (*yaani Super speciality*) na tunao wahitimu **saba (7)** ambao watatunukiwa shahada za uzamivu.

### **Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,**

Chuo kimeendelea kutekeleza malengo na majukumu yake kupitia Skuli, Kurugenzi na Taasisi zake. Kwa mwaka huu napenda kutaja mambo machache yaliyotekelezwa na Chuo kama ifuatavyo:-

#### **1. Kurugenzi ya Shahada za Awali (*Undergraduate Education*)**

Kwa mwaka huu wa masomo 2016/2017 Chuo kupitia Kurugenzi ya Shahada za Awali kimedahili wanafunzi **393** wa shaahada ya kwanza ambao ni asilimia 65.5 kwa waliodahiliwa mwaka wa masomo 2015/2016, na wanafunzi **268** wa stashahada ambao ni asilimia 45.6 ya wale waliodahiliwa mwaka wa masomo 2015/2016. Kupunguza udahili kunasababishwa na msonagamano mkubwa wa wanafunzi katika Chuo, kutokana na mundo mbinu finyu iliyopo katika Kampasi ya Chuo ya Muhimbili kwa sasa, na vile vile Uchache wa Rsilimali Watu unaosababisha Uwiano Usioridhisha wa Mhadhiri na wanafunzi. Hii vile vile utekelezaji wa mapendekezo ya

Kamati ya Baraza la pamoja la Madaktari na Madaktari wa Kinywa na Meno la Afrika Mashariki (*East African Community (EAC) Joint Medical and Dental Practitioners Councils/Boards*), iliyo agiza Chuo Kupunguza msongamano wa Wanafunzi na Kuboresha uwiano kati ya Mhadhiri na Wanafunzi.

## **2. Skuli ya Tiba**

Kwa mwaka wa masomo wa 2015/2016 Chuo kupitia Skuli ya Tiba kiliingia Mikataba ya Makubaliano yaani (*Memorandum of Understanding*) mitatu yenye lengo ya kuongeza ushirikiano katika Nyanja za kutoa elimu, mafunzo na tafiti. Mikataba hio ilikuwa kati ya Chuo kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na *Alliance for Global Clinical Training (AGCT)*, Chuo Kiku Cha Maharashtra Ch Sayanzi za Afya (*Maharashtra University of Health Sciences*) Nashik, India na Chuo Kikuu Cha Heildelberg (*Heidelberg University*). Makubaliano haya yatawezesha wanataaluma kusomea fani mbalimbali za tiba na kuongeza uwezo wa kutibu magojwa mbalimbali ikiwemo saratani.

## **3. Skuli ya Afya ya Kinywa na Meno**

Chuo Kupitia Skuli ya meno kimeendelea kutafuta njia mbalimbali za kuongeza mapato ya ndani. Kwa mwaka huu wa masomo Chuo kupitia Skuli ya Meno kimekamilisha ukarabati wa kliniki mpya ya wagonjwa wa meno watakao kuwa wanajilipia wenyewe. Vifaa vitakavyofunga kwenye klinikii hii vimeshapatikana kupitia ufadhili wa Shirika lisilo la Kiserikali la *The Miracle Corners of the World (MCW)* la New York Marekani na vinategemewa kuwasili nchini na kufungwa kwenye kliniki hiyo mnamo mwezi wa Januari mwakani. Matumaini yetu ni kwamba klinikii hii itakapoanza kufanya kazi itakiongezea Chuo Makusanyo ya mapato ya ndani, kwa kiasi kikubwa. Napenda kuchukua nafasi hii kushukuru Shirika hili la *The Miracle Corners of the World (MCW)* kwa ufadhili huo.

## **4. Skuli ya Famasia**

Katika Mwaka wa masomo wa 2015/2016, Chuo kupitia Skuli ya Famasia, kitengo cha Maabara ya Utafiti na Uhakiki wa Dawa (Pharm R&D Lab) kimeendeleza ushirikiano na Shirika la kusimamia viwango na upimaji la Ujerumani (*Physikalich Technische Bundesantalt - PTB*). Hivyo Maabara hii ilijengewa uwezo wa kutoa huduma ya ustadi wa kupima

sampuli za dawa za binadamu kimaabara (*Proficiency Testing Provider*) kwa ukanda wote wa Afrika ya Mashariki. Vile vile Chuo kupitia Skuli hii kinashirikiana na SUMA JKT katika kuanzisha kiwanda cha kutengeneza dawa za maji maji ya intravenous (*intravenous fluids*) katika eneo la Mgulani JKT.

## **5. Skuli ya Afya na Sayansi za Jamii**

Kwa Mwaka wa Masomo 2015/2016, Chuo kupitia Skuli ya Afya na Sayansi za Jamii kimeanzisha idara ya *Bio-ethics*. Idara hii itatoa mafunzo na ushauri hususani katika maadili ya tafiti za binadamu na huduma kwa ujumla.

Vile vile Chuo kupitia Skuli ya Afya na sayansi za Jamii kimeshirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto, kutengeneza mpango mkakati wa kuangalia afya ya wafanyakazi hususani wafanyakazi wa afya. Hii itawawezesha wafanyakazi kutambua afya zao na kuchukua hatua stahiki kabla madhara hayajatokea.

Chuo kimeshirikiana na Shirika la afya duniani (WHO) kuandaa mwongozo wa mafunzo ya kuelimisha wafanyakazi wa afya jinsi ya kutambua na kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya tabia nchi yanayoathiri afya ya binadamu. Hii itasaidia kupunguza athari za afya zinazotokana na mabadiliko ya tabi aya nchi.

## **6. Skuli ya Uuuguzi**

Ili kuharakisha mipango ya serikali ya kupunguza vifo vya kina mama na watoto, Chuo kupitia Skuli ya Uuguzi katika mwaka wa wamasomo wa 2015/16 kimetoa wahitimu tisa (9) kwa mara ya kwanza katika Shahada ya Uzamili ya Ukunga na Afya ya Wanawake yaani *Master of Midwifery and Women's Health*. Wahitimu hawa watakuwa ni viongozi na walimu katika kuboresha huduma za afya ya mama na watoto nchini.

## **7. Kurugenzi ya Mafunzo ya Uzamili na Uzamivu**

Chuo kupitia Kurugenzi ya Mafunzo ya Uzamili na Uzamivu kimeendelea kudahili wanafunzi kulingana na mahitaji ya wataalam katika sekta ya afya nchini. Hata hivyo, si wanafunzi wote wanaodahiliwa huweza kufanya usajili na kujiunga na masomo. Mfano, waliofanya usajili kati

ya waliodahiliwa kwa mwaka wa masomo 2014/15 ni 261 kati ya 469 (55.6%); mwaka wa masomo 2015/16 ni 354 kati ya 529 (66.9%); na mwaka huu wa masomo 2016/17 ni 256 kati ya 427 (59.9%). Kati ya wanafunzi waliodahiliwa, wale waliopata udhamini kutoka Serikalini kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika mwaka wa masomo 2014/15 ni 64 (18%); mwaka wa masomo 2015/16 ni 70 (27%); na mwaka wa masomo 2016/17 ni 90 (35%). Hivyo, Serikali imeonyesha jitihada za kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopewa udhamini. Tunaishukuru Serikali kwa jitihadi hizi, na kuomba ongezeko zaidi la idadi ya wanafunzi wanaopewa udhamini katika miaka ijayo kwani wengi wanaoshindwa kujiunga inawezekana inatokana na kukosa udhamini. Pia tunatoa wito kwa mashirika mbalimbali ya ndani na nje ya nchi kufadhili wanafunzi wa uzamili na uzamivu ili wanafunzi wengi waweze kupata na nafasi ya mafunzo hasa ukizingatia uhitaji mkubwa ulioko kwa wahitimu hawa nchini.

## **8. Kurugenzi ya Huduma za Maktaba**

Chuo kupitia Kurugenzi ya Huduma za Maktaba kimeendelea kutoa huduma za maktaba kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kuboresha huduma za ukusanyaji, utunzaji na usambazaji wa machapisho na majarida mbalimbali ya ki-elektroniki na kutoa mafunzo juu ya matumizi ya machapisho hayo kwa watumiaji wakiwemo walimu, wanafunzi na watafiti. Hata hivyo, sehemu kubwa ya huduma hizi imekuwa ikitegemea fedha za wahisani ambazo hazitoshelezi. Aidha tunapenda kutoa shukrani zetu kwa wahisani wanaoendelea kukifadhili Chuo ili kuboresha huduma za Kurugenzi ya Maktaba.

## **9. Kurugenzi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni muhimu katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wakati huu. Kwa mwaka wa masomo wa 2015/16, Chuo kupitia Kurugenzi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kimeendelea kuboresha matumizi ya TEHAMA kwa kupanua miundombinu na kuboresha utoaji wa huduma na ufanisi. Katika kipindi kilichopo sasa Chuo kupitia kurugenzi hii imetilia mkazo zaidi uboreshaji wa TEHAMA katika kutoa huduma na Kufundishia pamoja na ufunguja wa Miundo mbinu ya TEHAMA katika Hospitali ya



kufundishia fani za afya pamoja na kutoa Huduma ya Mloganzila ambayo shughuli zake zitategemea mifumo ya TEHAMA kwa asilimia kubwa, kwa kuwahusisha wataalamu wake katika mafunzo mbalimbali. Aidha Chuo bado kinatolea mkazo mkazo matumizi ya mifumo huru ya habari (*free and open source software system*) ili kupunguza gharama kubwa za kulipia leseni za mifumo katika juhudi za kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za Chuo.

## **10. Kurugenzi ya Masomo ya Kijiendeleza na Maendeleo ya Weledi**

Chuo kupitia Kurugenzi hii kimeendeleza mkakati wake wa kuratibu na kuendesha masomo ya kujiendeleza na warsha mbalimbali kwa wakufunzi (*Faculty Development Workshops*) wa Skuli, Taasisi na Idara mbali mbali hapa chuoni. Kwa mwaka huu wa masomo, Chuo kimeratibu kozi fupi mpya 12 zinazoendeshwa na vitengo mbali mbali hapa chuoni ili kuendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika sekta ya afya hapa nchini. Vile vile Chuo kimefanikiwa kukamilisha ujenzi wa jingo la Kituo cha Elimu za Taaluma za Afya (*Centre for Health Professions Education*) ambacho kinatarajiwa kuongeza nafasi zaidi katika kutoa mafunzo ya kujiendeleza na maabara za kuongeza umahiri (*Skills Labs*) kwa wafanyakazi na wanafunzi ili kufanikisha lengo la kutoa elimu bora na kuongeza ufanisi kwa wanafunzi na wafanyakazi waliyo kazini katika fani mbali mbali za afya. Aidha Chuo kinatoa shukrani kwa za dhati kwa Shirika la Bill na Melinda Gates (*The Bill and Melinda Gates Foundation*) lililowezesha kwa kiasi kikubwa kuanza kwa ujenzi wa Kituo hiki.

## **11. Kurugenzi ya Mipango na Uwekezaji, Kampasi ya Muhimbili**

Katika mwaka wa fedha wa 2015/16, chuo kupitia Kurugenzi ya Mipango na Uwekezaji, Kampasi ya Muhimbili kimeanza na kukamilisha mchakato wa kungia ubia na benki ya EXIM kujenga matawi yake katika eneo la kampasi ya Muhimbili na Mloganzila. Ujenzi huu ambao utafanyika kwa makubaliano ya *Build Operate and Transfer (BOT)*, utawezesha chuo kupata mapato kutokana na kodi ya pango kwa benki hiyo na baadae majengo hayo kuwa mali ya chuo. Matawi hayo ya benki yatasaidia kutoa huduma kwa wanajumuiya ya chuo ikiwemo kutoa mikopo nafuu kwa wanafunzi wa shahada mbalimbali wanaosoma hapa chuoni.

Kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi Chuoni kumekuwa na uhaba mkubwa sana wa hosteli za wanafunzi. Hosteli zilizopo katika kampasi ya Muhimbili ni za zamani sana na zinaingizia chuo hasara kubwa.

Mapato yanayopatikana katika hosteli hizo ni asilimia 43 tu ya gharama zinazotakiwa kukarabati hosteli hizi kila mwaka. Hivyo chuo kupitia Kurugenzi ya Mipango na Uwekezaji kinafanya jitihada za kutafuta wawekezaji binafsi watakaoweza kuingia ubia na Chuo ili kujenga hosteli za kisasa zinazokidhi mahitaji ya karne ya sasa. Hosteli hizi mpya zitatoa nafasi zaidi kwa wanafunzi wa ndani na pia kuweza kuvutia wanafunzi wa nje wanaotaka kujiunga na chuo. Aidha Chuo kimeanza kuunda Kampuni itakayoshughulikia shughuli zote za uwekezaji na kuongeza mapato ya Chuo (*MUHAS Holding Company*) baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Chuo.

## **12. Kurugenzi ya Mipango na Uwekezaji, Kampasi ya Mloganzila**

Katika mwaka wa masomo wa 2015/16, kupitia Kurugenzi yake ya Mipango na uwekezaji, Kampasi ya Mloganzila, Chuo kiliendelea na uendelezaji wa Kampasi hii mpya.

Kama alivyoeleza Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, ujenzi wa Kampasi ya Mloganzila ni muhimu sana ili Chuo kiweze kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 4000 wa sasa mpaka wanafunzi 15,000. Ujenzi wa Hospitali yenye vitanda 571 umekamilika na Jengo kukabidhiwa rasmi kwa Uongozi wa Chuo tarehe 13 Octoba, 2016. Vile vile Vifaa tiba vimeshafungwa katik Hospitali hii.

Kazi kubwa iliyobaki mbele yetu ni ujenzi wa majengo na miundombinu mingine ya Chuo katika Kampasi hii ya Mloganzila. Ili kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo na miundombinu ya kampasi hii, Chuo kimetayarisha dokezo sabili (*proposal*) ili kuainisha gharama halisi ya ujenzi wa kampasi hii itakayokuwa na kumbi za mihadhara, maabara za kufundishia, mabweni ya wanafunzi, jengo la utawala, nyumba za wafanyakazi, na miundombinu mingine muhimu ya kampasi ya chuo.

AVile vile, Chuo kimeandaa dokezo sabili lingine (*proposals*) kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya wanafunzi, hosteli za *interns*, na nyumba za wafanyakazi wa chuo. Jumla ya gharama za mradi huu ni takribani Dola za Kimarekani 320,199,835. Chuo kimefanya mazungumzo na Shirika la Nyumba la Taifa, Benki ya Uwekezaji ya Tanzania (*TIB Development Bank Ltd*) na Shirika la *Africa Integras* la Marekani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Mashirika haya yalionyesha nia ya kuwekeza katika huu mradi na kutaka kupataiwa ridhio ya serikali (*Government guarantee*) ili

waendeleo na ujenzi wa miundombinu hiyo.

Katika kupanua miundombinu ya Kampasi ya Chuo Mshauri Mwelekezi wa ujenzi wa kituo cha umahiri (consultant) ameshapatikana na mkataba umeshasainiwa kati na Uongozi wa Chuo tarehe 4 Agosti, 2016. Mkandarasi wa ujenzi anatarajiwa kupatikana mwezi January, 2016 baada ya kukamilisha michakato husika. Ni matumaini yetu kwamba serikali na wafadhili wengine wataona umuhimu wa ujenzi wa Kampasi hii mpya na kukisaidia chuo ili kupata rasilimali fedha kwa ajili ya kujenga majengo na miundombinu mingine ya Chuo iliyobaki na kibali cha kuajiri watumishi wanaokidhi kuendesha hospitali ya Chuo kwani watumishi 268 walipatiwa kibali kuajiriwa hawatoshi.

### **13. Kurugenzi ya Utafiti na Machapisho**

Utafiti ni moja ya nguzo tatu za Chuo chetu. Kwa kuzingatia umuhimu huu, Chuo kupitia Kurugenzi yake ya Utafiti na Machapisho kwa mwaka huu kimefanikiwa kuratibu miradi ya utafiti zaidi ya **71** inayoendelea hapa Chuoni. Vile vile idadi ya machapisho ya watafiti wa Chuo kwa mwaka 2015/16 ilikuwa ni jumla ya 579. Ikijumuisha majarida ya ndani na nje ya nchi, dissertations, conferences papers na vitabu. Hili ni ongezeko la asilimia 14.5 ukilinganisha na mwaka 2014/15 ambapo chuo kilitoa machapisho 495.

Aidha kwa asilimia kubwa tafiti hizi zinafadhiliwa kupitia wadau wa maendeleo (*development partners*) wa Chuo. Kwa mwaka huu Chuo kina jumla ya washiriki wa tafiti (*collaborators*) 35 kwa kutumia Taasisi za Ufadhili (donors) 61 ambazo zimekiwezesha Chuo kuendesha tafiti mbalimbali. Kwa mfano Shirika la maendeleo la Sweden-Sida limefandili tafiti mbalimbali tangu 1986; katika kipindi cha 2015-2020 Shirika hili la Sida limetoa Krona 82,000,000 sawa na Shilingi za Kitanzania 19,680,000,000 ili kukiwezesha chuo kusomesha wataalam 37 kwa ngazi ya uzamivu (PhD) na 23 kwa ngazi ya uzamili (MSc). Tafiti zimekuwa na mchango mkubwa katika kupata ufumbuzi wa matatizo mbalimbali ya afya yanayosumbua jamii ya watanzania na sehemu nyingine duniani. Kwa hiyo nachukua nafasi hii kuwapongeza watafiti wetu na kuwashukuru wadau wote wa maendeleo. Kipekee nichukue fursa hii kuishukuru Serikali yetu kwa kuweka mahusiano mazuri na wadau wa maendeleo pote

duniani ambayo imetuwekea mazingira mazuri ya ufadhili na ushirikiano wa kimataifa katika tafiti. Tunaiomba Serikali iendelee kuunga mkono na kuchangia katika shughuli za utafiti katika nchi yetu kwa ujumla.

#### **14. Kurugenzi ya Rasilimali Watu na Utawala**

Chuo Kupitia Kurugenzi ya Usimamizi wa Rasilimali Watu na Utawala katika mwaka 2015/16 kiliendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia masuala ya Rasilimali Watu na kuratibu masuala mbalimbali ya maendeleo ya Chuo na watumishi ili kuhakikisha kwamba Chuo kinafikia malengo yake ambayo ni kufundisha, kufanya Tafiti na Ushauri. Hata hivyo Upungufu wa wafanyakazi katika ngazi mbalimbali bado ni tatizo kubwa linaloathiri ufanisi wa Chuo katika utekelezaji wa majukumu yake. Kwa sasa mahitaji halisi ya wafanyakazi ni kama 1,700 lakini wafanyakazi walioko ni 637 tu, kati yao wanataaluma ni 304. Hii ni nusu ya mahitaji halisi ya rasilimali watu hapa Chuoni. Vile vile ili Hospitali ya Mloganzila ifanye kazi kwa ufanisi tunahitaji wafanyakazi wa kuanzia 928. Chuo kinaishukuru Serikali kwa kutoa kibali cha ajira mpya 50 na zingine 213 zitakazojazwa kwa njia ya uhamisho. Hata hivyo hii ni asilimia 28 tu ya mahitaji halisi ya kuendesha Hospitali hii ya Chuo ya kufundishia na kutoa huduma. Hivyo Chuo kitaendelea kushauriana na serikali kupitia ofisi ya Utumishi wa Umma, Wizara wa Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kukabiliana na upungufu huo.

#### **15. Taasisi ya Madawa ya Asili**

Chuo kupitia Taasisi ya Madawa Asili kimeendelea kutoa mafunzo kwa waganga na watoa huduma za tiba asilia. Lengo la mafunzo haya ni kuendeleza na kukuza weledi ili kuboresha huduma za tiba za waganga kama inavyoelekezwa na sheria ya tiba asili na tiba mbadala ya mwaka 2002, maelekezo ya sera ya Afya ya Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya mwaka 1990, pamoja na miongozo inayotolewa na shirika la afya duniani (WHO) kanda ya Afrika.

Aidha katika juhudi za kuongeza wigo wa mapato yatakayo saidia kazi za utafiti kwa mwaka huu Chuo kupitia Taasisi hii imesaini makubaliano na asasi binafsi ya Cloud 9 Wellness Services kwa nia ya kusambaza bidhaa

zake za ngozi. Vile vile Chuo kupitia Taasisi hii kimeendelea kufanya tafiti za kuboresha bidhaa zinazotokana na mitidawa ya asili, ambapo mchakato wa kusajili bidhaa kwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) umekamilika na hivyo kufanya Taasisi kuwa na bidhaa 4 ambazo zinaweza kusambazwa ndani na nje ya nchi.

### **Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,**

Kwa kumalizia napenda kuwapongeza tena wote waanao hitimu leo na kuwatakiya mafanikio mema katika shughuli zenu mtakazoenda kuzifanya za kujenga Taifa. Hongereni sana na ni matumani yangu kwamba wengi wenu mtarudi tena hapa Chuoni kwa ajili ya masomo ya juu zaidi ili kujiongezea ujuzi na weledi katika fani zenu. Kama ilivyo kawaida tunategemea mtaendelea kuwa mabalozi wazuri wa Chuo hiki, popote pale mtakapokuwa.

Mwisho kabisa naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa wanataaluma wote na wafanyakazi wengine wa Chuo hiki kwa kushiriki kikamilifu na kuhakikisha kwamba wanafunzi hawa wanaohitimu na wengine wote wa Chuo hiki wanapata elimu itakayowawezesha kutekeleza majukumu yao huko waendako.

### **Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, wageni waalikwa, mabibi na mabwana,**

Asanteni kwa kunisikiliza na nawatakieni maadhimisho mema ya Krismasi na Mwaka Mpya wa 2017.

**MWISHO**

**03 Desemba, 2016.**







**CHUO KIKUU CHA AFYA  
NA SAYANSI SHIRIKISHI, MUHIMBILI**

**Ofisi ya Naibu**  
Makamu Mkuu wa Chuo  
Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaaluma,  
Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili,  
S.L.P. 65001,  
DAR ES SALAAM.

